

Umuhimu wa Kupata Dozi Yako ya Pili ya Nakala ya Chanjo ya COVID-19

[muziki wa kuchangamsha]

[Kris Ehresmann] Hujambo jina langu ni Kris Ehresmann na mimi ni mkurugenzi wa magonjwa ya kuambukiza katika Idara ya Afya ya Minnesota. Ningependa kuzungumza nanyi leo kuhusu umuhimu wa chanjo lenu la pili la COVID-19.

Kwa chanjo zinazopatikana za COVID-19, zingine zinahitaji dozi mbili. Mtu anayekupa chanjo yako atakujulisha ikiwa unahitaji dozi ya pili, na ikiwa unahitaji dozi mbili, ujumbe huu ni wako.

Chanjo zote zinazopatikana za COVID-19 ni salama na zinafaa kwa hivyo unapaswa kupokea chanjo yoyote utakayopewa. Kwa chanjo za COVID-19 ambazo zina dozi mbili, ni muhimu kupokea dozi zote mbili kwa kinga bora dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Kumbuka, dozi zote zinahitaji kuwa aina moja ya bidhaa ya chanjo. Dozi hupeanwa zikiachana na wiki tatu hadi nne kulingana na chanjo ya dozi mbili unayopata.

Unapopata dozi yako ya kwanza ya chanjo, unapaswa kufanya miadi ya dozi ya pili. Ni wazo nzuri kuiandika kwenye kalenda yako au kuiweka kwenye simu yako ili kukusaidia kukumbuka.

Kunaweza kuwa na hali ambapo mtu hawezi kupata dozi ya pili kwa wakati unaofaa. Hiyo ni sawa. Tunataka kukuhimiza ujaribu na kupata miadi ya dozi ya pili haraka iwezekanavyo. Huna haja ya kuanza tena msururu wa chanjo.

Ingawa kumekuwa na habari zinazoahidi uwepo wa ulinzi kutoka kwa dozi moja ya bidhaa ya dozi mbili, bado kuna mengi tunayohitaji kujifunza. FDA bado inapendekeza dozi mbili za chanjo hizi na kupokea dozi zote mbili za chanjo ya dozi mbili ya COVID-19 inahakikisha kuwa una kinga bora dhidi ya ugonjwa.

Asante kwa kupata chanjo. Kila mtu anayepata chanjo hutuleta hatua moja karibu na kuangamiza COVID.

[muziki unaocheza]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

3/10/21 (Swahili)

Ili kupata maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989